

# HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA



## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA IMEPOKEA KIBALI CHA AJIRA YA WATUMISHI WAWILI WA KADA YA WASAIDIZI WA HESABU WATAKAOFANYA KAZI KATIKA KITUO CHA AFYA IGOMA (MMOJA) NA MAKONGORO (MMOJA) KWA LENGU LA KUIMARISHA USIMAMIZI WA FEDHA KATIKA VITUO HIVYO KUENZIA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 AMBAPO VITUO HIVYO VITAPOKEA FEDHA ZOTE ZINAZOHUSU HUDUMA ZA AFYA KUTOKA SERIKALI KUU NA WADAU WA MAENDELEO.

- AJIRA HIZI ZITAKUWA ZA MKATABA WA MWAKA MMOJA MMOJA KWA KUZINGATIA KIPINDI CHOTE AMBACHO WAFADHILI WATAGHARAMIA AJIRA ZAO. KIPINDI CHA UFADHILI KIKIMALIZIKA WATUMISHI HAWA HAWATAINGIZWA MOJA KWA MOJA KATIKA UTARATIBU WA AJIRA ZA SERIKALI BALI ITATEGEMEA UFANISI NA UTENDAJI KAZI WAO.
- AIDHA, AJIRA ZA WATUMISHI HAWA ZINAWEZA KUENDELEA BAADA YA MIKATABA YAO KWISHA KWA MASHARTI YA MIKATABA KWA MISHAHARA INAYOTOKANA NA MALIPO YA MAKUSANYO YA NDANI YA VITUO HUSIKA AU KUTOKA KATIKA HALMASHAURI HUSIKA.

KUTOKANA NA KIBALI HICHO MKURUGENZI WA JIJI ANAWATANGAZIA NAFASI ZA KAZI KAMA IFUATAVYO:

### **SIFA ZA UJUMLA: MWOMBAJI WA NAFASI YA KAZI ANATAKIWA:**

1. AWE RAIWA WA TANZANIA.
2. AWE NA ELIMU YA KIDATO CHA IV (NNE) NA KUENDELEA.
3. AWE NA UMRI KATI YA MIAKA 20 – 40.

4. AWE NA UWEZO KUFANYA KAZI ATAKAZOPANGIWA NA MKUU WAKE WA KAZI.
5. MAOMBI YAAMBATANE NA VIVULI VYA VYETI VYA SHULE NA TAALUMA PAMOJA NA MAELEZO BINAFSI (CV).
6. AWE HAJAWAHI KUHUKUMIWA KWA KOSA LOLOTE LA JINAI (CRIMINAL OFFENCES).
7. AWE AMERIDHIA KIASI CHA MALIPO KITAKACHOTOLEWA KWA KAZI HII.
8. WAOMBAJI WOTE WAWA NA AFYA NJEMA, HAIBA NA WENYE MAADILI MEMA KUTUMIKIA UMMA.

### **NAFASI ZA KAZI:**

### **MSAIDIZI WA HESABU (ACCOUNTS ASSISTANT) - NAFASI 2**

#### **KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA HESABU:**

- KUANDIKA NA KUTUNZA "REGISTER" ZINAZOHUSU SHUGHULI ZA UHASIBU.
- KUANDIKA HATI ZA MALIPO NA HATI ZA MAPOKEZI YA FEDHA.
- KUTUNZA MAJALADA YENYE KUMBUKUMBU ZA HESABU.
- KUPELEKA BARUA/NYARAKA ZA UHASIBU BENKI.
- KUFANYA USULUHISHO WA MASURUFU, KARADHA, HESABU ZA BENKI NA AMANA.

#### **UWAJIBIKAJI:**

MSAIDIZI WA HESABU ATAWAJIBIKA KWA MGANGA MFAWIDHI WA KITUO.

#### **SIFA:**

CHETI CHA "ATEC LEVEL II" AU "FOUNDATION LEVEL" KINACHOTOLEWA NA NBAA, WAOMBAJI WAWA NA UZOEFU WA KAZI ZAIDI YA MWAKA MMOJA (1) KATIKA FANI HIYO.

#### **NGAZI YA MSHAHARA:**

NGAZI YA MSHAHARA ITAKUWA TGS B, KIMA CHA KUENZIA NI SHILINGI 390,000/=.

#### **NAMNA YA KUTUMA MAOMBI:**

MAOMBI YOTE YAANDIKWE KWA MKONO, NA YAAMBATANISHWE NA NAKALA ZA VYETI PAMOJA NA NAKALA YA MAELEZO BINAFSI

(CV) AMBAYO IMECHAPWA KWA MASHINE AU KOMPYUTA NA KUSAINIWA NA MWOMBAJI. MAOMBI YATUMWE KWA ANWANI IFUATAYO:

**MKURUGENZI WA JIJI,  
HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA,  
S.L.P 1333,  
MWANZA**

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI NI TAREHE 24/07/2017 SAA TISA NA NUSU ALASIRI (09:30)

**OMARY ISMAIL KAMATA  
KAIMU MKURUGENZI WA JIJI**